



HeartKids

Ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa: Sababu

Maelezo juu ya sababu za ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa.

Ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa ni nini?

Ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa (Congenital heart disease – CHD) ni neno la jumla kwa hali mbalimbali zinazoathiri jinsi moyo unavyofanya kazi.

Congenital ina maana kuwa hali ipo tangu kuzaliwa. Ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa ni aina ya kawaida sana ya kasoro ya kuzaliwa. Mtoto 1 kati ya watoto 100 huzaliwa na kasoro ya moyo.¹

KATI YA KESI 8 YA 10
ZA UGONJWA WA
MOYO ZA MTOTO



SABABU HAIJULIKANI²

Ni nini inayosababisha ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa?

Katika takriban 80% ya kesi za ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa sababu haijulikani.

Baadhi ya akina mama wa watoto wachanga waliozaliwa na ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa wanaangalia kwa makini tabia zao wakati wa ujauzito kujaribu kupata sababu. Ni muhimu kukumbuka kuwa kesi nyingi za ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa hazina sababu inayojulikana.

Baadhi ya sababu zinazojulikana za ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa ni:

- **Jenetiki.** 20% ya kesi zina sababu ya kijenetiki.²
- **Magonjwa wakati wa ujauzito.** Magonjwa kama vile surua ya Ujermani yanaweza kuongeza hatari ya ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa.
- **Matibabu.** Matibabu fulani yanaweza kuongeza hatari ya mama kupata mtoto mwenye ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa kama yakitumiwa wakati wa ujauzito.
- **Umri.** Watoto wa wanawake wa umri mkubwa wanawezekana kuwa na kasoro ya kuzaliwa kuliko watoto wa wanawake wadogo zaidi.



- **Kasoro nyingine za kuzaliwa.** Mtoto mwenye Ugonjwa wa Down Syndrome anawezekana zaidi kuwa na kasoro ya moyo.
- **Kuvuta sigara, kunywa pombe au kutumia dawa za kulevya wakati wa ujauzito.**
- **Ugonjwa wa kisukari au lishe duni wakati wa ujauzito.**

Je, itatokea tena katika familia yetu?

Takriban 1% ya watoto wanazaliwa na ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa.¹ Hatari ya itatokea tena katika familia yako inatofautiana kutegemea hali yako na aina ya ugonjwa.

Tunajua kwamba:

- Ikiwa tayari una mtoto mwenye ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa lakini huna historia yoyote ya ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa katika familia yako, hatari yako ya kupata mtoto mwingine mwenye ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa inaongeza kidogo kuwa takriban 3 hadi 4 %.
- Ikiwa zaidi ya ndugu mmoja wana ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa, hatari ya kupata mtoto mwingine mwenye ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa inaongezeka
- Hatari ya kupata mtoto mwenye ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa inaongezeka kama mmoja wa wazazi ana ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa. Iwapo mama ni mzazi aliyeathirika, hatari kuwa ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa unapitisha kwa watoto ni juu zaidi²

Iwapo una ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa na unawaza kuanza kupata watoto, labda utakuwa na maswali kwa daktari wako kuhusu vipimo vya kijenetiki. Anaweza kutoa ushauri kuhusu hali yako na mwelekezo kwa huduma ya ushauri wa kijenetiki ikifaa.



Katika kesi nyingi, sababu haijulikani, inayoweza kupunguza chaguzi kwa vipimo vya kijeni.

Ushauri nasaha wa kijenetiki ni nini?

Huduma za ushauri wa kijeni hutoa maelezo kwa watu na familia ambao wanazo, au wapo hatarini ya kupata, kasoro fulani za kuzaliwa.

Iwapo jeni zilisababisha ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa na madaktari wanaweza kutambua jeni zipi, ni rahisi zaidi kutabiri kiasi gani itakawezekana kwamba itatokea kwa mwanafamilia mwingine au mtoto.

Katika baadhi ya kesi, wanaweza kutoa maelezo ya kina kuhusu sababu zinazoweza na hatari za kasoro kutokea tena.

Zungumza na daktari wako juu ya ushauri wa kijeni na kama utakuwa chaguo nzuri kwako.

Marejeo

¹ VAN DER LINDE, D., KONINGS, E., SLAGER, M., WITSENBURG, M., HELBING, W., TAKKENBERG, and J. J. & ROOS-HESELINK (2011). "Birth prevalence of congenital heart disease worldwide: a systematic review and meta-analysis." *Journal of the American College of Cardiology*. 58: 2241-2247.

² BLUE, G. M., KIRK, E. P., SHOLLER, G. P., HARVEY, R. P. & WINLAW, D. S. (2012). "Winlaw DS. Congenital heart disease: current knowledge about causes and inheritance." *The Medical Journal of Australia* 197: 155- 159.


Karatasi hii ya ukweli ilikaguliwa na kusasishwa na HeartKids mwezi Machi 2021. Iliidhinishwa na Kamati yetu ya Ushauri wa Kliniki wakati wa kuchapishwa. Taarifa za kliniki zinaweza kubadilika baada ya tarehe hii. Taarifa katika karatasi hii ya ukweli ni ya jumla. Sio mbadala wa ushauri wa kimatibabu kutoka kwa daktari wako. Wakati wote zungumza na daktari wako kuhusu mambo yanayoathiri afya yako.

Mahali pa kupata maelezo zaidi na usaidizi.

HeartKids

 heartkids.org.au

Jifunze zaidi juu ya ugonjwa wa moyo wa kuzaliwa na msaada ambayo HeartKids inaweza kukuofa.

 1800 432 785

Piga simu kwa Simu ya Msaada ya HeartKids kwa usaidizi, ushauri na mwongozo.

 @HeartKidsAustralia

 @HeartKids